# TAARIFA YA MAFANIKIO YA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA MIAKA 60 (1964- 2024) YA MAPINDUZI MATUKUFU YA ZANZIBAR KATIKA UTEKELEZAJI WA AHADI ZA SERIKALI

## UTANGULIZI

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilianzishwa rasmi mwaka 2010 kufuatia marekebisho ya 11 ya Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984, iliyoruhusu kuwepo na kuanzishwa Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Ibara ya 39 (5) ya Katiba ya Zanzibar ya 1984 inaelekeza kuwepo kwa Makamu wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar ambaye atakuwa Mshauri Mkuu wa Rais katika kutekeleza kazi zake.

Kimuundo Ofisi hii, inaongozwa na Makamu wa Kwanza wa Rais ambaye anasaidiwa na Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Mtendaji Mkuu wa Ofisi ni Katibu Mkuu ambaye anasaidiwa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kupitia wakuu wa Taasisi na Idara.

## UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Katika utekelezaji wa majukumu yake, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inatumia miongozo mbalimbali ya Serikali ikiwemo Dira ya Maendeleo ya zanzibar ya 2050, Mpango wa Maendeleo ya Zanzibar wa mwaka 2021 – 2026, Sera, Sheria, Kanuni na Mpango Mkakati

wa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Ilani ya Uchanguzi ya CCM ya 2020 - 2025. Aidha, Ofisi inasimamia Sera nne ambazo ni Sera ya Mazingira ya 2013, Sera ya Watu wenye Ulemavu ya 2018, Sera ya VVU na UKIMWI ya 2012 na Sera ya Kudhibiti na Kupambana na dawa za Kulevya ya 2023. Kwa upande wa Sheria, Jumla ya Sheria tano zinasimamiwa na Ofisi hii ambazo ni Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Namb. 3 ya 2015, Sheria ya Uanzishwaji wa Tume ya UKIMWI Namb. 3 ya 2002, Sheria ya Kusimamia na Kukinga Masuala ya UKIMWI Namb. 18 ya 2013, Sheria ya Watu wenye Ulemavu Namb. 8 ya 2022, Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Namb. 8 ya 2021.

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaundwa na Taasisi tatu zinazojitegemea ambazo ni Tume ya UKIMWI, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) na Idara sita zilizopo chini ya Katibu Mkuu ni Ofisi ya Faragha, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti, Idara ya Uendeshaji na Utumishi, Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, Idara ya Mazingira na Ofisi Kuu Pemba.

Ofisi ya Faragha ndio yenye dhamana ya kusimamia na kuhakikisha kazi na shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais zinafanyika kwa ufanisi mkubwa.

## SEKTA ZA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jumla ya sekta kuu nne ambazo ni Sekta ya usimamizi wa Mazingira, Sekta ya usimamizi wa Dawa za kulevya, Sekta ya usimamizi wa Watu wenye ulemavu na Sekta ya usimamizi wa UKIMWI.

## A. SEKTA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA

Sekta hii inajumuisha Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA). Idara ya Mazingira ilianzishwa mwaka 1989 chini ya iliyokuwa Kamisheni ya Ardhi na Mazingira ndani ya Ofisi ya Waziri Kiongozi (1989 – 1990). Aidha, mwaka 1990, Idara ya Mazingira ndani ya Kamisheni ya Ardhi na Mazingira ilihamishiwa Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati, Ardhi na Mazingira.

Mwaka 1992, Sera ya kwanza ya Mazingira ilianzishwa na kufuatiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira na Maendeleo Endelevu namba 2 ya mwaka 1996. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, Idara ya Mazingira ilikuwa na majukumu yote mawili ya utawala wa mazingira, utekelezaji na uzingatiaji wa Sheria ya mazingira.

Mwaka 2000, Idara ya Mazingira ilihamishiwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mazingira na Ushirika hadi mwaka 2010 (2000 – 2010). Mwaka 2010, Idara ya Mazingira ilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais hadi mwaka 2016.

Mwaka 2013, Sera ya pili ya Mazingira ilitayarishwa ambayo ilifuatiwa na Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 3 ya mwaka 2015. Marekebisho hayo ya Sheria yaliwezesha kuwepo kwa Idara ya Mazingira ambayo pamoja na mambo mengine majukumu yake ya msingi ni utawala wa mazingira ikiwa ni pamoja na kutayarisha mikakati na miongozo ya kitaifa ya usimamizi wa mazingira na kuratibu utekelezaji wake; kuratibu utekelezaji wa mikataba ya kimataifa na kikanda ya kimazingira; kuratibu masuala ya mabadiliko ya tabianchi ikiwa ni pamoja na shughuli za kuhimili na kukabiliana na athari za mabadiliko hayo; kuendeleza elimu ya mazingira kwa jamii na wadau wengine kwa mujibu wa majukumu yake; na kuratibu na kuendeleza utafiti wa kimazingira.

Mwaka 2015, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira Zanzibar (ZEMA) ilianzishwa chini ya kifungu cha 14(1) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira namba 3 ya mwaka 2015 chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Kazi za msingi za ZEMA zimetajwa kwenye kifungu cha 22(1). Miongoni mwa kazi hizo ni kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sheria ya mazingira; kuratibu hatua za Tathmini za Athari za Kimazingira na ukaguzi wa kimazingira kwa shughuli mbalimbali au uwekezaji; kufanya ufuatiliaji wa kimazingira ambao utasaidia kuendeleza usimamizi bora na uhifadhi wa mazingira; kutekeleza kanuni na kuhakikisha uzingatiaji wa viwango, miongozo na amri kuhusiana na mazingira; kufuatilia bioanuwai, mifumo ya ikolojia ya nchi kavu na baharini, ukanda wa pwani, utupaji wa taka na maji machafu na maliasili; kupokea na kuyafanyia kazi malalamiko yanayohusiana na mazingira; na kuendeleza elimu ya

mazingira, ufahamu, na usambazaji wa taarifa kwa jamii na wadau wengine zinazohusiana na kazi za Mamlaka.

Mwaka 2016, Idara ya Mazingira na ZEMA zilihamishiwa Wizara ya Ardhi, Maji, Nishati, na Mazingira hadi mwaka 2017. Aidha, mwaka 2017, taasisi hizo zilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais hadi mwaka 2021 ambapo zilihamishiwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Hadi sasa, Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira zipo chini ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais.

Kwa kipindi cha miaka 60 ya Mapinduzi ya Zanzibar ya Mwaka 1964, Sekta ya Mazingira imepata mafanikio mbalimbali. Miongoni mwa mafanikio hayo ni:

1. Kufanikiwa kuondoa wastani wa tani 360 za kemikali hatarishi zilizomaliza muda wa matumizi ambazo zilikuwa zimehifadhiwa katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kemikali hizo zililetwa kwa ajili ya matumizi ya afya, kilimo, viwanda na matumizi ya maabara ya Skuli. Kemikali hizo zimekusanywa na kupelekwa Uingereza kwa ajili ya uangamizaji ulio salama kwa mazingira na afya ya jamii.

2. Kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambayo ilikuwa ni tishio kwa uharibifu na uchafuzi wa mazingira pamoja na afya kwa jamii. Mafanikio makubwa yamepatikana katika udhibiti wa mifuko hiyo na kupelekea Zanzibar kuwa miongoni mwa nchi za kupigiwa mfano katika suala la udhibiti wa mifuko ya plastiki. Kwa ujumla, mifuko

ya plastiki imepungua kuzagaa mitaani kama ilivyokuwa imezoeleka siku za nyuma.

3. Serikali imeendelea kuhakikisha kuwa miradi ya kiuchumi na maendeleo inayoanzishwa Zanzibar inazingatia usimamizi wa mazingira kwa kufanya tathmini za athari za kimazingira; na ukaguzi wa kimazingira. Kuanzia mwaka 2015/2016 hadi Disemba, 2023, jumla ya miradi 642 imefanyiwa tathmini za kimazingira. Aidha, miradi 34 imefanyiwa Tathmini ya athari za kimazingira mwaka 2015/2016 na miradi 136 imefanyiwa mwaka 2022/2023 ambapo kumekuwa na ongezekeo la miradi 102. Ongezeko hili linatokana na juhudi za Serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais za kuhakikisha kuwa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inazingatia masuala ya mazingira wakati wa uanzishwaji na utekelezaji wa miradi hiyo. Aidha, vyeti vya kimazingira hutolewa kwenye miradi hiyo ambavyo huambatanishwa na masharti ya kimazingira na vyeti hivyo kwa ajili ya kuhakikisha kuwa miradi hiyo inaendeshwa bila ya kuwa na uharibifu na uchafuzi mkubwa wa mazingira.

4. Serikali imefanikiwa kujenga mtambo wa kusafisha maji machafu katika eneo la Msingini Chake Chake Pemba pamoja na msingi wa kupitisha maji ya Mvua wenye urefu wa mita mia moja (100) katika eneo hilo. Kuwepo kwa mtambo huo kunasaidia kupunguza utiririshaji wa maji machafu na hatimae uchafuzi wa mazingira ya bahari ya Hifadhi ya Mkondo wa Pemba.

5. Katika juhudi za kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imefanikiwa kuandaa na kuzindua Mkakati wa Zanzibar wa

Mabadiliko ya Tabianchi wa mwaka 2014 ambao unatoa dira ya hatua za Serikali na wadau zinazotakiwa kuchukuliwa za kuhimili na athari za mabadiliko ya tabianchi. Imefanikiwa kuyarejesha baadhi ya maeneo yalioathirika na mabadiliko ya tabianchi kutokana na mmong'onyoko wa fukwe na uingiaji wa maji ya chumvi katika maeneo ya kilimo na makaazi. Jumla ya hekta 337 za mikoko zimepandwa katika maeneo yanayoingia maji ya chumvi ya Kilimani, Kisakasaka, Tovuni, Ukele, Kisiwa Panza na Tumbe. Aidha, kuta na matuta ya kuzuia maji ya bahari kupanda juu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mpango wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zimejengwa kwa baadhi ya maeneo ya Unguja na Pemba. Baadhi ya sehemu zilizojengwa matuta ni Tumbe West (250m); Ukele (700m); Sizini (200m); Mziwanda (400m); Gando Nduuni (150m); Chokaani (20m); Kengeja (120m).

6. Kuta mbili (2) zenye jumla ya urefu wa mita 50 zimejengwa katika eneo la Kisiwa Panza Pemba na kuta tano (5) za aina ya "groynes" zenye jumla ya mita 420 zimejengwa katika eneo la Kilimani. Aidha, ukuta wenye urefu wa mita 300 umejengwa katika eneo la bahari ya Mizingani Forodhani chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango. Ukuta huo umesaidia katika kuulinda na kuuhifadhi Mji Mkongwe wa Zanzibar ambao umo kwenye Urithi wa Kimataifa unaotambuliwa na UNESCO.

   Pia Serikali imefanikiwa kujenga ukuta wenye urefu wa mita 49 katika eneo la Likoni Kojani, Pemba, ukuta wenye urefu wa mita 500 katika eneo la Msuka, na tuta lenye urefu wa mita 400 katika eneo

la Tovuni. Serikali inaendelea kujenga madaraja mawili katika eneo la Sipwese, Mkoani Pemba, moja lina urefu wa mita 225 na jengine mita 120. Ujenzi wa madaraja hayounafanyikwa kwa mashirikiano na serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

7. Katika juhudi za kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi, Serikali imefanikiwa kujenga ukuta wenye urefu wa mita 49 katika eneo la Likoni Kojani, Pemba, ukuta wenye urefu wa mita 500 katika eneo la Msuka, na tuta lenye urefu wa mita 400 katika eneo la Tovuni. Yote hayo yamejengwa kwa ajili ya kunusuru na kuzuia mmgong'onyoko wa fukwe katika maeneo hayo. Kujenga kwa kuta na tuta hilo kumewawezesha wananchi wa maeneo hayo kuendelea na shughuli zao za kiuchumi na kijamii zilizokuwa zimeathirika na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Serikali pia imefanikiwa kuchimba visima sita virefu pamoja na ujenzi wa minara ya kuhifadhia matangi ya maji katika maeneo ya Matemwe, Unguja. Pia imenunua boti sita (6) za aina ya fiber pamoja na injini zake na mitego ya kuvulia samaki ambazo wamepatiwa wanajamii wa Matemwe katika shehia ya Kijini, Jugakuu na Mbuyutende ikiwa ni sehemu ya kuhimili athari za mabadiliko ya tabainchi.

8. Serikali imefanikiwa kuongeza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia vipindi vya redio na TV, mikutano, na mitandao ya kijamii. Aidha, kutokana na elimu hiyo, kumekuwa na mwamko mkubwa wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya maeneo yetu na pia umepelekea kuongezeka kwa Asasi za kiraia za utunzaji na uhifadhi

wa mazingira pamoja na klabu za uhifadhi wa mazingira katika Skuli za Msingi na Sekondari Unguja na Pemba. Vikundi vya mazingira vimeongezeka kutoka 67 mwaka 2022 hadi kufika 73 mwaka 2023.

9. Serikali pia imefanikiwa kuingiza masuala ya mazingira kwenye mitaala ya Skuli pamoja na kuanzisha Vilabu vya Mazingira vya Skuli. Jumla ya Vilabu 53 vya Mazingira vimeansihwa katika Skuli mbali mbali Unguja na Pemba kwa lengo la kukuza uelewa na umuhimu wa uhifadhi na usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa wanafunzi wa Skuli hizo.

10. Serikali imeandaa miongozo miwili ya kimazingira ambayo ni (1) Muongozo wa Uanzishaji na Uendelezaji wa Viwanda vya kusaga mawe, kifusi na utengenezaji wa matofali. Lengo kuu la muongozo huo ni kutoa maelekezo ya kimazingira ya kuanzisha, kuendesha na kusimamia viwanda vinavyosaga mawe na kifusi pamoja na kuchekecha kifusi na kokoto Zanzibar ili viwe endelevu na visiwe na athari kubwa za kimazingira na kero kwa jamii. (2) Muongozo wa Ufuatiliaji wa Kimazingira kwa ajili ya Hoteli za Kitalii. Muongozo huo umeandaliwa kwa lengo la kuziwezesha Hoteli za kitalii kuweza kufanya ufuatiliaji binafsi katika utunzaji wa mazingira pamoja na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kuweza kufuatilia Hoteli hizo ili kuimarisha utunzaji wa mazingira kwa kushajihisha utalii endelevu katika visiwa vya Zanzibar.

11. Serikali imefanikiwa kuongeza uelewa na ushiriki wa jamii katika utunzaji na uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kupitia vipindi vya redio na TV, mikutano, na mitandao ya

kijamii. Aidha, kutokana na elimu hiyo, kumekuwa na mwamko mkubwa wa kulinda na kuhifadhi mazingira ya maeneo yetu na pia umepelekea kuongezeka kwa Asasi za kiraia za utunzaji na uhifadhi wa mazingira pamoja na klabu za uhifadhi wa mazingira katika Skuli za Msingi na Sekondari Unguja na Pemba. Vikundi vya mazingira vimeongezeka kutoka 67 mwaka 2022 hadi kufika 73 mwaka 2023.

## B. SEKTA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA

Katika sekta hii juhudi za kupambana na kudhibiti dawa za kulevya zilianza hapa Zanzibar kabla ya Mapinduzi mnamo mwaka 1915 chini ya usimamizi wa Sheria ya *Abuse of Opiates Decree No. 5 ya1915*.

Aidha, juhudi hizo zilendelea baada ya Mapinduzi ya mwaka 1964 hadi kufikia mwaka 2003 ambapo ilianzishwa Idara ya Kupambana na Dawa za Kulevya chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa Sheria No. 16 ya 2003 kwa Sheria iliyofahamika kama ni “the Drugs and Prevention of Illicit Traffic Drugs Act”.

Mnamo mwaka 2009 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, lilitunga na kupitisha Sheria mpya No. 9 ya 2009 iliyojulikana kama sheria ya kudhibiti dawa za kulevya ambayo ilipelekea kuanzishwa kwa taasisi mpya iliyojuilkana kama Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya.

Pia kufuatia marekebisho ya Katiba ya Zanzibar iliyopelekea kuleta mageuzi ya Serikali katika uendeshaji wake mwaka 2010 ilipelekea kuanzishwa kwa Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ambapo taasisi hii iliwekwa chini ya ofisi hiyo.

Katika kukabiliana na janga hili thakili linaloharibu nguvu kazi nchini, Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dr. Hussein Ali Mwinyi katika mazungumzo yake na kituo cha Azam TV alipotimiza siku 100 za uongozi wake aliadhimia kwa makusudi na kwa mustakabali wa nchi yetu, kufanya mabadiliko makubwa kwenye tasnia ya kudhibiti dawa za kulevya, ikiwemo kuifuta Sheria ya Udhibiti na Usafirishaji wa Dawa za Kulevya, Nam. 9 ya mwaka 2009 na kutunga Sheria mpya inayoendana na kasi ya sasa ya mapambano dhidi ya dawa za kulevya pamoja na Kuanzisha Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, yenye uwezo kamili wa kukabiliana na uhalifu huu.

Katika kufikia dhamira ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, mwaka 2021 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitunga Sheria Mpya inayojulikana kama "Sheria ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya 2021" ambayo ndio imeweza kuleta mageuzi katika suala hili na kupewa uwezo wa Kisheria wa kuchunguza, kukamata, kupeleleza na kupeleka mahkamani mashauri yote yanayohusiana na dawa za kulevya na makosa yanayofanana nayo.

Kiujumla katika mapambano hayo, Ofisi ya makamu wa Kwanza wa Rais kupitia Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya imeweza kupata mafanikio yafuatayo;

1. Kutoa elimu na kuelimisha jamii juu ya athari za matumizi ya dawa za kulevya. Katika hili tumefanikiwa kukutana na Masheha wa shehia za Wilaya zote za Unguja na baadhi ya Shehia za Pemba kwa lengo la kujadili mikakati na mbinu mbalimbali za udhibiti wa dawa za kulevya katika shehia zao. Aidha, tumekua tukitoa elimu kupitia vyombo vya habari mbali mbali vya Redio na Televisheni ikiwemo ZBC TV na Redio pamoja na mitandao ya kijamii. Lakini kwa vile waathirika wakubwa wa dawa za kulevya ni vijana tumeweza kuzifikia skuli mbalimbali za Unguja na Pemba kwa lengo la kuwapatia elimu wanafunzi na walimu juu ya athari ya matumizi ya dawa za kulevya.

2. Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya tabia kilichopo Kidimni ambacho ni kitovu cha malezi ya vijana walioathirika na matumizi ya Dawa za Kulevya, katika kituo hichi vijana wetu hawa wanapatiwa tiba sahihi na stadi za maisha kama vile ufugaji kuku na ng’ombe, ushoni, kilimo cha mboga (green house) na gereji ya kisasa kwa lengo la kuwapatia elimu ya ujasiriamali vijana waliokubali kuachana na matumizi ya dawa za kulevya waliopo katika kituo hicho. Jumla ya vijana 48 wanaendelea kupatiwa matibabu na marekebisho ya tabia Kati ya vijana hao, vijana 15 wameshaunganishwa na mafunzo ya ujasiriamali kupitia miradi iliyoanzishwa katika kituo hicho.

## C. SEKTA YA USIMAMIZI WA WATU WENYE ULEMAVU

Sekta hii ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar, inajumuisha masuala ya Haki za Watu wenye Ulemavu ambayo yalianza mara tu baada ya Mapinduzi matukufu ya mwaka 1964. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilitambua ustawi wa Watu wenye Ulemavu na kuhakikisha wanapata huduma za kijamii, kiuchumi haki na fursa sawa ikiwemo fursa za uongozi katika ngazi mbalimbali.

Juhudi binafsi za wananchi kuhusu masuala ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar zilianza kuonekana mwanzoni mwa miaka ya1980, ambapo mwaka 1985 Umoja wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar (UWZ) ulianzishwa rasmi. Kwa upande wa Serikali, masuala ya Watu wenye Ulemavu yaliratibiwa rasmi mwaka 1986 na yaliwekwa kwenye Idara ya Ustawi wa Jamii iliyokuwa chini ya Wizara ya Afya. Mwaka 2000 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyahamishia masuala ya Watu wenye Ulemavu katika iliyokuwa Ofisi ya Waziri Kiongozi kwa lengo la kuleta msukumo zaidi katika kusimamia masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa vile Ofisi hii ndiyo iliyokuwa na jukumu la kuratibu shughuli zote za Serikali.

Serikali ilitunga Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004, kwa lengo la kuweka utaratibu wa kisera katika kusimamia na kuongoza utekelezaji wa shughuli zinazohusiana na masuala ya Watu wenye Ulemavu Zanzibar iliyopelekea kutungwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu Nam 9 (Haki na Fursa) 2006.

Aidha, kutokana mabadiliko ya uchumi, Teknolojia, tamaduni, mawazo chanya ilipelekea kutungwa Sera mpya ya Watu wenye Ulemavu mwaka 2018 baada ya kugundua mapungufu yasiyokidhi mahitaji kwa sasa na ndio sababu zilizopelekea kufanya mapitio ya Sheria ya Watu wenye Ulemavu ya mwaka 2006 kwa lengo la kuimarisha utoaji na usimamizi wa huduma kwa wananchi. Kufuatia mabadiliko hayo, sekta ya Watu wenye Ulemavu imeweza kupata mafanikio yafuatayo;

1. Kutungwa kwa Sheria ya Watu wenye Ulemavu namba 8 ya mwaka 2022. Chini ya sheria hii, Watu wenye Ulemavu watapatiwa fursa zitakazowawezesha kufikia na kushiriki kikamilifu katika shughuli za kijamii kwa kujitegemea na kuwaondoshea ubaguzi kutokana na ulemavu wao.

2. Kuanzishwa kwa mfumo wa Kielektroniki wa ukusanyaji wa taarifa za Watu wenye Ulemavu ambapo jumla ya watu 16,492 wameweza kusajiliwa na kutambuliwa kwa hatua za awali.

3. Jumla ya vifaa saidizi 6821 vya aina mbalimbali vilitolewa kwa Watu wenye Ulemavu ambapo Unguja 3,412 na Pemba 3,409. Vifaa hivyo vinajumuisha viti vya magurudumu mawili, fimbo nyeupe, miwani, magongo ya kwapani, magongo ya kutembelea, lotion na kofia, baskeli za maguridumu matatu.

4. Jumla ya Watu wenye Ulemavu 127 wamewezeshwa ambapo waliopatiwa mikopo ni 86, elimu 23 na matibabu 18

5. Uanzishwaji wa mabaraza ya Watu wenye Ulemavu kwa Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa lengo la kuwatambua Watu wenye

Ulemavu, mahitaji yao na kuhakikisha haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu zinapatikana katika ngazi za Wilaya.

## D. SEKTA YAKURATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI

Tume ya UKIMWI Zanzibar ni Taasisi iliyoazishwa kwa Sheria Namba 3 ya mwaka 2002. Jukumu kubwa la Tume ya UKIMWI ni kuratibu na kusimamia mikakati ya kudhibiti maradhi ya UKIMWI hapa Zanzibar. Kihistoria, Tume ya UKIMWI ilianzishwa mwaka 2002 chini ya Ofisi ya Waziri Kiongozi. Kabla ya kuanzishwa kwa Tume jukumu la kusimamia mapambano dhidi ya maradhi ya UKIMWI lilikuwa chini ya Wizara ya Afya katika Kitengo cha Kudhibiti UKIMWI. Kitengo hicho kilianzishwa mwaka 1987 kufuatia kugundulika kwa wagonjwa watatu wa mwanzo wenye maradhi ya UKIMWI Visiwani Zanzibar mwaka 1986 katika hospitali ya Mnazi Mmoja.

Shughuli za kupambana na maradhi ya UKIMWI zilikuwa zikitekelezwa kwa kuzingatia Mipango Mikakati ya miaka mitano mitano iliyokuwa ikijulikana kama “Medium Term Plans” (MTPs). Jumla ya Mikakati (MTPs) mitatu ilitekelezwa baina ya mwaka 1987 hadi mwaka 2002.

Baada ya kuanzishwa kwa Tume ya UKIMWI shughuli za UKIMWI zikaanza kutekelezwa kwa kuzingatia Mkakati wa Taifa wa Kupambana na UKIMWI (National HIV/AIDS Strategic Plans) badala ya MTPs. Mikakati hii imekuja kuendeleza yale yote yaliyokuwa

yakisimamiwa kupitia MTPs zilizopita pamoja na kuongeza juhudi za kupatikana kwa dawa kwa watu wanaoishi na Virusi vya UKIMWI (VVU), kuanzisha huduma za kumlinda mtoto asipate maambukizo ya VVU kutoka kwa mama mjamzito mwenye maambukizo ya VVU, kupiga vita unyayapaa katika jamii na sehemu za kazi, kuzijengea uwezo taasisi binafsi ili kuisaidia Serikali katika mapambano dhidi ya UKIMWI, kuimarisha mfumo wa utunzaji taarifa na kufanya tafiti mbalimbali kwa ajili ya kufuatilia mwenendo wa maradhi ya UKIMWI katika jamii.

Kwa ujumala katika kutekeleza majukumu, Tume ya UKIMWI Zanzibar imeweza kupata mafanikio mbalimbali. Miongoni mwa mafanikio hayo ni;

1. Tume kwa kushirikiana na wadau mbali mbali imefanikiwa kupunguza maambukizo mapya ya Virusi vya UKIMWI kutoka watu 499 waliopata maambukizo mapya mwaka 2012 hadi watu 117 kwa mwaka 2023.
2. Kupunguza vifo vinavyotokana na maradhi ya UKIMWI kutoka vifo 682 mwaka 2012 hadi vifo 107 mwaka 2023.
3. Kwa kushirikiana na wadau mbali mbali tumefanikiwa kudhibiti kiwango cha watu wanaoishi na VVU na kuendelea kubaki kuwa chini ya asilimia 1. Utafiti wa mwaka huu 2023 umeonesha Zanzibar tuna asilimia 0.4 ya watu ambao wanaishi na Virusi vya UKIMWI
4. Kwa kushirikiana na wadau mbali mbali tumeweza kupunguza kiwango cha unyanyapaa kwa watu wanaoishi na Virusi vya

UKIMWI, kutoka asilimia 56 mwaka 2004 hadi asilimia 31 mwaka 2023.

5. Kufanya tafiti mbali mbali zilizowezesha kufahamu mwenendo wa maradhi haya katika nchi yetu.

**MWELEKEO WA OFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS**

1. Kuifanya Zanzibar kuwa ya kijani kwa kuhakikisha inapanda miti kwa lengo la kulinda na kuhifadhi mazingira katika jamii na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi chini ya Mpango wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani (Green Legacy Program)
2. Kuendelea kuhakikisha kuwa miradi ya kiuchumi na kimazingira inazingatia masuala ya mazingira pamoja na kuimarisha ufuatiliaji wa kimazingira kwa ajili kulinda na kuhifadhi mazingira yetu.
3. Kuendeleza maeneo yaliyoathiwa na mabadiliko ya tabianchi ili kuiwezesha Zanzibar kujilinda na kujihami na athari za mabadiliko hayo.
4. Kujenga kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Pemba pamoja na kuongeza juhudi katika utoaji wa tiba, kwa waathirika wa dawa za kulevya na kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha
5. Kuendelea na ujenzi wa vituo vya wajasiriamali kwa watu wenye ulemavu ili kuwawezesha kiuchumi Unguja na Pemba

6. Kuendelea kufanya tafiti zinazohusiana na hali halisi ya watu wenye ulemavu, mabadiliko ya tabianchi na athari za kimazingira pamoja na dawa za kulevya hapa nchini.
7. Kuendelea kufanya mapitio ya Sheria, kanuni na Sera zote za Wizara zilizobakia ili kuhakikisha kwamba tunakwenda sambamba na kasi ya mabadiliko ya awamu ya nane.
8. Kuimarisha zoezi la ufuatiliaji na tathmini ya majukumu ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ikiwemo hali ya UKIMWI Zanzibar na vihatarishi vyake hasa kwa watu wenye ulemavu, vijana na akina mama.
9. Kuendelea kukuza na kuimarisha mashirikiano baina ya SMT, SMZ na taasisi mbalimbali za ndani na nje pamoja na washirika wa maendeleo.
10. Kuendelea kutekeleza mikakati ya kupambana na mikakati ya UKIMWI ili tufikie shabaha za 95 tatu mwaka 2025, ambazo ni shabaha za msingi za kumalizika tatizo la ukimwi ifikapo 2030.
11. Kuhakikisha masuala ya Watu wenye Ulemavu yanazingatiwa katika sera sheria na programu mbali mbali za ofisi.